

## 1. UTANGULIZI

Darubini ya Dira ya Taifa ni taarifa inayotoa tathmini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ambayo ilianzwa kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongoza harakati za maendeleo ya uchumi na jamii zitakazoiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na umasikini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Taarifa hii itakuwa ikitolewa mara nne kila mwaka, ikiwa inalenga kuwahabarisha wataanzania katika ngazi zote hadi vijijini, kuhusu juhudi zinazofanywa na serikali kutekeleza mipango ya kimaendeleo kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Kila toleo litakuwa likielezea utekelezaji wa lengo moja au mawili ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

## 2. MALENGO MAKUU MATANO YALIYOAINISHWA KWENYE DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

Darubini ya Dira inachambua mafanikio pamoja na changamoto zinazoikabili nchi ya Tanzania katika kufikia malengo makuu matano yaliyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Malengo hayo ni: (i) Kuboresha hali ya maisha ya wataanzania; (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani, usalama na umoja; (iii) Kujenga utawala bora; (iv) Kuwepo jamii iliyoelimika vyema na inayojifunza; na (v) Kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine. Ili kutimiza malengo hayo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuboresha viashiria muhimu vya uchumi, kama vile kuchochea ukuaji wa pato la taifa, kushusha mfumuko wa bei, kuvutia wawekezaji kutoka nje, kupunguza ukosefu wa ajira n.k pamoja na kuendeleza sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

## 3. MIPANGO MBALIMBALI ILIYOANDALIWA KUTEKELEZA MALENGO MAKUU MATANO

### 3.1 Mpango waMaboresho ya Utumishi wa Umma

Mpango huu wamaboresho ya utumishi wa umma ni mojawapo ya mipango ya awali iliyoandaliwa na serikali ikiwa na nia ya kutimiza malengo ya Dira ya Taifa kufikia mwaka 2025. Lengo kuu la mpango huo ni kuongeza ubora na ufanisi wa kutenda kazi katika Wizara mbalimbali, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na Sekretarieti za Mikoa. Mpango huo ulio chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma umekuwa ukitekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza (2000-2007) ililenga uanzishwaji wa mifumo bora ya usimamizi wa utendaji wa watumishi wa umma. Awamu ya pili (2008-2012) ilikuwa na dhumuni la kuimarisha utendaji na uwajibikaji. Awamu ya tatu (2012-2017) inaazimia kuongeza ubora wa kazi zinazofanywa na watumishi wa umma. Mfumo mzuri wa utumishi wa umma unachangia kujenga utawala bora unaosimamia vyema matumizi ya rasilimali za taifa kwa manufaa ya wote, hivyo kuboresha hali ya maisha ya watu, kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

### 3.2 Malengo ya Maendeleo ya Millenia

Katika harakati za kupambana na umaskini, wakuu wa nchi zinazounda Umoja wa Mataifa walikutana nchini Marekani mwaka 2000 na kuweka maazimio ya pamoja ya kutekeleza malengo nane (8) ya maendeleo ifikapo mwaka 2015. Malengo hayo, yanayoitwa *Malengo ya Maendeleo ya Millenia*, ambayo kila nchi haina budi kuyatekeleza ni: (i) Kuondokana na umaskini wa kipato na njaa; (ii) Kutoa elimu ya msingi kwa watoto wote; (iii) Kuweka usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake (iv) Kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano; (v) Kuboresha huduma za afya ya uzazi; (vi) Kudhibiti UKIMWI, malaria na magonjwa mengineyo (vii) Kuhakikisha uwepo wa mazingira endelevu; na (viii) Kuendeleza mshikamano wa kimataifa katika masuala ya maendeleo. Malengo haya yote yanatekelezwa kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 pamoja

na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA).

### 3.3 Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA)

Ili kufikia malengo ya kimaendeleo ya nchi, serikali iliandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA I, 2005-2010 uliofuatiwa na MKUKUTA II, 2010-15) ikiwa ni mikakati ya muda wa kati wa kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na pia kuweza kufikia Malengo ya Millennia ambayo ni malengo yaliyokubalika kimataifa kwa ajili ya kupunguza umaskini. MKUKUTA umeundwa na nguzo kuu tatu ambazo ni (i) Kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini, (ii) Kuboresha hali ya maisha na (iii) Kuhakikisha uwepo wa utawala bora pamoja na uwajibikaji. MKUKUTA umegusa masuala muhimu kama vile elimu, afya, ajira, makazi, mazingira na usawa wa kijinsia. Mkakati huo umeazimia, pia kuongeza ushiriki wa wanajamii katika kutunga na kuhuisha sera na sheria pia kutilia mkazo wa kuondoa tamaduni zinazorudisha nyuma maendeleo. Malengo ya MKUKUTA yatafanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kadri Serikali itakavyokuwa inaendeleo kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wote, kama Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma unavyoelekeza.

Hata hivyo, katika mipango hiyo ya awali hakukuwa na mfumo rasmi linganishi wa utayarishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango ya muda wa kati na muda mrefu, ili kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ili kurekebisha pengohilo, Serikali iliamua kuandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (miaka 15) ulioanza mwaka 2011/12.

### 3.4 Mpango Elekezi wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka 15

Mpango huu ni njiamuhimuya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kwa kuwa umeweka wazi mwelekeo wa kimkakati kwa muda mrefu na nguzo kuu kwa ajili ya umakini zaidi, uratibuna kuoanishamipango iliyowekwa, ili kuleta maendeleo. Utekelezaji wake utafanyika kwa vipindi vitatu

vya muda wa kati wa miaka mitano mitano hadi mwaka 2025. Lengo kuu la kipindi cha kwanza cha mpango huu ni kutumia vizuri rasilimali za nchi, ili kuondokana na umaskini. Maeneo ya kipaumbele na kimkakati yaliyoainishwa kwa mwaka 2011/12-2015/16 ni: kuboresha miundombinu ya usafiri, nishati na maji; kilimo; viwanda; maendeleo ya rasilimali watu; na huduma za jamii. Kipindi cha pili cha mpango huo (2016/17-2020/21) kitabeba dhana ya kujenga uchumi unaotegemea viwanda wakati kipindi cha tatu (2021/22-2025/26) kitalenga ongezeko la ushindani kuwezesha bidhaa zinazozalishwa nchini kuuzwa nje ya nchi.

### 3.5 Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16)

Mpango huu ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango elekezi wa muda mrefu. Tayari mpango huu uliobeba dhana ya kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi upo kwenye hatua ya utekelezaji. Lengo kuu la kipindi cha kwanza cha mpango huu ni kutumia vizuri rasilimali za nchi ili kujikwamua na umaskini. Maeneo ya kipaumbele na kimkakati yaliyoainishwa kwa mwaka 2011/12-2015/16 ni kuboresha miundombinu ya usafiri, nishati na maji, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii. Malengo ya mpango huu wa miaka mitano yameoainishwa na yale ya MKUKUTA I na MKUKUTA II ambayo yataliwezesha taifa kufikia Malengo ya Millenia na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

### 3.6 Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/13

Kipindi cha kwanza cha Mpango wa Miaka Mitano kimeanza kufanyika kupitia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/13, ambao unazingatia vipaumbele vilivyotajwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16), MKUKUTA, Malengo ya Millenia 2015 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Mpango wa mwaka 2012/13 uliainisha miradi katika maeneo yenye fursa kubwa za kukuza uchumi na kuleta

maendeleo ya kijamii. Mradi mmojawapo katika mpango huo ni ujenzi wa Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini, ambacho kitakuwa kitovu cha biashara na huduma kwa nchi za maziwa makuu. Pia, miradi mingine ilielekezwa katika uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji itakayoiwezesha Tanzania kuwa njia kuu ya biashara ya usafirishaji kwa za nchi jirani. Utekelezaji wamiradi hiyo unafanyika kupitia bajeti ya Serikali ya maendeleo kwa mwaka 2012/13 na 2013/14.

### 3.7 Mkakati wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa

Kwa kutambua umuhimu wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi, programu na mikakati ya maendeleo, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Serikali kupitia wizara mbalimbali imeweka mkakati mpya uitwao 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' ambao umejikita katika kuchambua kwa kina programu na miradi ya kipaumbele iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao umelenga katika kuainisha maeneo machache yatakayoweza kuleta matokeo makubwa kwa haraka ifikapo mwaka 2025. Serikali imechagua sekta muhimu sita, ambazo zitaanza kutumia mfumo huo mpya ambazo ni kilimo, nishati, elimu, upatikanaji wa rasilimali fedha na usafiri,, hususan uboreshaji wabandari ya Dar es Salaam pamoja nareli ya kati. Ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mfumo huu utakuwa ukifanyika chini ya uratibu na usimamizi wa Ofisi ya Rais, ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yanafikiwa.

## Economic and Social Research Foundation (ESRF)

P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania.  
Phone: (+255) 754 780 133, (+255) 777 790 133,  
(+255) 782 780 133 • Fax: (+255 22) 2760062  
E-mail: esrf@esrf.or.tz • Website: www.esrf.or.tz



# DARUBINI YA DIRA YA TAIFA 2025

